# PBPA Bulletin

**TOLEO Na. 01 | MACHI, 2025**





# Wakala wa Uagizaji wa Mafuta Kwa Pamoja: Suluhisho la Kupunguza Gharama za Mafuta Nchini



Katika miaka ya hivi karibuni, sekta ya mafuta nchini Tanzania imepitia mageuzi makubwa yaliyolenga kuleta ufanisi, uwazi, na upatikanaji wa mafuta kwa gharama nafuu. Hatua muhimu katika mageuzi haya ilikuwa kuanzishwa kwa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (Petroleum Bulk Procurement Agency - PBPA), taasisi iliyoleta mwangaza katika sekta iliyowahi kukumbwa na changamoto nyingi.

## Mwanzo wa Mabadiliko

Miaka ya 2000 ilileta mfumo wa soko huria, ambapo makampuni ya mafuta yalipewa uhuru wa kuagiza mafuta moja kwa moja kutoka soko la dunia na kupanga bei zake kulingana na mwenendo wa soko. Ingawa mfumo huu ulileta wawekezaji wapya, ulikuwa pia na changamoto nyingi, zikiwemo udanganyifu wa bei, aina ya mafuta na ukosefu wa uwekezaji katika miundombinu.

Kwa nyakati tofauti, nchi ilikumbwa na changamoto ya upatikanaji wa mafuta, mlundikano wa meli bandarini na gharama kubwa zisizoendana na uhalisia wa soko na kuchanganya Mafuta ya taa na dizeli. Hali hii ilipelekea hasara kubwa kwa wananchi pamoja na Serikali kukosa mapato stahiki.

## Kuzaliwa kwa Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja

Ili kutatua matatizo haya, Serikali ilipitisha Sheria ya Petroli ya mwaka 2008, ambayo ilisisitiza umuhimu wa kuwa na mfumo wa ununuzi wa mafuta ulio bora na wenye uwazi. Hatua hii ilifanikiwa mwaka 2012 kwa kuanzishwa mfumo uliokuwa chini ya PIC na baadae mwaka 2015 PBPA ilipewa jukumu hilo kama taasisi ya Serikali.

Kwa mujibu wa kanuni za Petroli za mwaka 2011, PBPA ilipewa mamlaka ya kuhakikisha kuwa mafuta yote yanayoingia nchini yanaagizwa kwa ufanisi na ushindani ulio wazi. Hatua iliyosaidia kudhibiti bei, kupunguza gharama zisizo za lazima, na kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha kwa wakati wote.

## Matunda ya Mfumo Mpya

Faida za mfumo huu zimekuwa dhahiri. Tangu kuanzishwa kwake, PBPA imefanikiwa kupunguza gharama za uagizaji mafuta kwa wastani wa dola milioni 200 za Kimarekani kwa mwaka, jambo linalofaidisha walaji wa kawaida na biashara kubwa na ndogo.

Gharama za meli kusubiria bandarini malipo yanayotokana na ucheleweshaji wa meli bandarini zimepungua kwa dola milioni 170 kwa mwaka, kwani mfumo wa uagizaji wa pamoja umewezesha mafuta kuagizwa kwa shehena kubwa na kupakuliwa kwa haraka zaidi.

Serikali pia imenufaika kwa ongezeko la mapato yatokanayo na kodi ya mafuta, huku nchi jirani zisizo na bandari kama Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) zikianza kutumia bandari za Tanzania kuingiza mafuta yao, hivyo kuongeza mapato ya taifa.

## Udhibiti wa Ubora na Ufanisi

Katika kuhakikisha kuwa mafuta yanayopatikana nchini yana ubora unaostahili, taasisi kama Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Vipimo (WMA) zimepewa jukumu la kuyakagua kabla ya kuingizwa nchini Aidha, Serikali imefunga mita za kidijitali (flow meters) katika bandari za Dar es Salaam, Mtwara, na Tanga, zinazowezesha mafuta kupimwa kwa usahihi ili kudhibiti upotevu na wizi.

Mfumo wa SCADA unafanya kazi saa 24 kwa siku wakati wa upakuaji wa mafuta, kuhakikisha kuwa hakuna mafuta yanayopotea. Matokeo yake ni kuokolewa kwa wastani wa tani 1,100 za mafuta kila mwezi.

## Changamoto na Mustakabali wa Sekta

Pamoja na mafanikio haya, bado kuna changamoto zinazoikumba sekta ya mafuta nchini. Baadhi ya changamoto hizi ni pamoja na hitaji la kuwekeza zaidi katika miundombinu ya mafuta ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka, pamoja na kuhakikisha kuwa mfumo huu unatoa manufaa ya muda mrefu kwa Watanzania wote.

Serikali, kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi, inaendelea kufanya kazi kwa karibu kuhakikisha kwamba mfumo huu unaboreshwa zaidi. Uwazi, usimamizi madhubuti, na uwekezaji katika teknolojia ya kisasa vitahakikisha kuwa sekta ya mafuta nchini Tanzania inazidi kuwa thabiti na yenye manufaa kwa uchumi wa taifa.

Katika safari hii ya mageuzi, PBPA imethibitisha kuwa mfumo wa uagizaji wa pamoja ni nyenzo muhimu ya kudhibiti soko la mafuta kwa ufanisi, huku ikihakikisha kuwa wananchi wanapata bidhaa hii muhimu kwa bei nafuu na kwa uhakika wa upatikanaji.



*Picha ya Pamoja ya Wajumbe Kamati ya Zabuni ya Mfumo wa Uagizaji Mafuta (BPS) na Washindi wa zabuni ya ununuzi wa mafuta kwaajili ya matumizi ya Mwezi Machi, 2025.*

# Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (BPS): Hatua Muhimu katika Kuimarisha Usambazaji wa Mafuta kwa Gharama Nafuu

Katika juhudi za kuhakikisha upatikanaji wa mafuta kwa gharama nafuu na ufanisi mkubwa, Serikali kupitia Wizara ya Nishati ilianzisha Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta wa Pamoja (BPS) chini ya sheria ya Petroli ya mwaka 2011 na kuanza kufanya kazi rasmi mwaka 2015 chini ya usimamizi na uangalizi wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA).

Mfumo huu unalenga kuongeza uwazi, kuimarisha ushindani wa haki, na kupunguza gharama za mafuta nchini. Ili Kampuni ya Mafuta iweze kuingia kwenye mfumo wa BPS inapaswa kuwasilisha nyaraka mbalimbali kuomba usajili kwa Wakala, ikiwa ni pamoja na barua ya maombi, leseni, vyeti vya usajili,taarifa za fedha na uthibitisho wa hifadhi ya mafuta pamoja na kuingia mkataba wa uingizaji mafuta na PBPA kabla ya kushiriki kwenye zabuni ya BPS kama muagizaji wa mafuta.

## Mchakato wa Zabuni: Uwazi na Ushindani wa Haki

Mchakato wa ununuzi wa mafuta kupitia mfumo wa BPS unafuata hatua maalum kuhakikisha uagizaji wa bidhaa za mafuta unakuwa wa haki na wenye gharama nafuu. Kwa mujibu wa mwongozo mpya, ni kampuni zilizoorodheshwa awali pekee ndizo zinazostahili kushiriki katika zabuni za ununuzi wa mafuta.

Kampuni za Masoko ya Mafuta (OMCs) zinapaswa kuwa na leseni halali ya uuzaji wa jumla wa mafuta kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ili kushiriki katika mfumo huu.

Katika mchakato wa kufuzu, wasambazaji wa mafuta wanapaswa kuwasilisha nyaraka muhimu kama vile leseni za biashara, taarifa za kifedha, na rekodi za uzoefu katika sekta ya mafuta. Wasambazaji wanaokidhi vigezo hupewa vibali vya kushiriki katika zabuni kwa kipindi cha miaka mitatu.

Zabuni hutangazwa kupitia magazeti ya kitaifa na kimataifa, tovuti rasmi ya PBPA, barua pepe kwa wasambazaji waliowahi kufuzu, na balozi za Tanzania nje ya nchi. Tangazo linajumuisha maelezo muhimu kama aina ya mafuta yanayohitajika, muda wa kujaza zabuni, na masharti ya usambazaji.

## Uchambuzi wa Zabuni na Utoaji wa Mikataba

Wasambazaji wa mafuta waliohitimu hutuma dondoo za zabuni kwa PBPA ndani ya muda uliopangwa. Kila dondoo lazima ijumuishe masharti ya kifedha na uthibitisho wa uwezo wa kusambaza mafuta. PBPA hufanya uchambuzi wa dondoo zote kwa uwazi, huku majina ya kampuni zinazoshiriki yakitangazwa hadharani. Mshindi wa zabuni ni anayetoa bei ya chini zaidi huku akikidhi mahitaji ya ubora wa mafuta kulingana na viwango vya Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Mshindi wa zabuni hupewa mkataba wa kusambaza mafuta kulingana na mahitaji yaliyoainishwa.

Baada ya kushinda zabuni, mshindi hupanga uagizaji wa mafuta kwa mujibu wa mkataba wake na PBPA. Mafuta huwasili katika kituo maalum cha mapokezi kinachojulikana kama Single Receiving Terminal Operator. Baada ya ukaguzi wa ubora, mafuta husambazwa kwa Kampuni za Uagizaji Mafuta (OMCs) kulingana na mahitaji yao.

## Uhakika wa Upatikanaji wa Mafuta kwa Wananchi

PBPA inahakikisha upatikanaji wa mafuta kwa wananchi kupitia, Tathmini ya mahitaji ya soko kwa kutumia taarifa za mauzo na historia ya uagizaji wa mafuta, Makadirio ya uagizaji mafuta kwa miezi sita yanayotolewa OMCs ili kuwezesha upangaji wa mahitaji ya kitaifa.


Kwa kuhakikisha uwazi na ushindani wa haki, PBPA huendelea kuchapisha matangazo ya maombi ya kufuzu kwa usambazaji wa mafuta kwenye magazeti ya kitaifa na kimataifa, tovuti yake rasmi, na kupitia Balozi za Tanzania duniani kote.


## Mwelekeo wa Baadaye wa Sekta ya Mafuta

Mfumo wa BPS unalenga kupunguza gharama za mafuta kwa wananchi na sekta mbalimbali za uchumi, Kuhakikisha upatikanaji wa mafuta wa uhakika kwa watumiaji wa ndani na viwanda na Kuimarisha uwazi na ushindani katika sekta ya mafuta nchini.

Kupitia mfumo huu wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja, Tanzania itaendelea kuboresha sekta yake ya mafuta, kuhakikisha bidhaa hii muhimu inapatikana kwa urahisi, kwa bei nafuu, na kwa uwazi wa hali ya juu.

Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (BPS) umethibitisha kuwa nyenzo muhimu katika kuhakikisha upatikanaji wa mafuta kwa gharama nafuu. Uwazi na ushindani katika zabuni umeleta manufaa makubwa kwa sekta ya nishati, huku Serikali ikiendelea kutekeleza hatua zaidi za kuboresha mfumo huu kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa.




*Mwakilishi wa Kampuni ya Mafuta akiweka maombi ya zabuni kwenye boski la zabuni*





*Meneja wa Mipango ya Mafuta Bw. Gilbert Jungulu akifunga sanduku la maombi ya zabuni ya ununuzi wa mafuta kwaajili ya matumizi ya Mwezi Machi, 2025.*



*Bw. Ali Saeed, Mwenyekiti wa Kamati ya Zabuni ya Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja (BPS), akifungua zabuni za ununuzi wa mafuta kwa matumizi ya Machi 2025.*

*Meneja wa Uendeshaji na Ugavi Bw. Raymond Lusekelo akitoa neno la Ufunguzi wa mchakato wa zabuni ya ununuzi wa mafuta kwaajili ya matumizi ya Mwezi Aprili, 2025.*





*Mhasibu Devotha Kachumita akipitisha moja ya dondoo za zabuni za kampuni kwa washiriki wa zabuni hiyo kuashiria uwazi katika kuendesha mchakato huo.*

*Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Zabuni ya Mfumo wa Uagizaji Mafuta (BPS) wakiendela na mchakato wa zabuni ya ununuzi wa mafuta kwaajili ya matumizi ya Mwezi Machi, 2025.*





# PBPA Yashauri Ujenzi wa Matenki ya Mafuta Bandari ya Mbamba Bay

***Wajumbe wa Bodi ya Ushauri PBPA wakipata maelezo ujenzi wa Bandari ya Mbamba Bay – Wilaya ya Mbinga kutoka kwa Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa Manga Gasaya (wa pili kulia).***

Bodi ya Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) imeishauri Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kuangalia uwezekano wa kujenga maghala ya kuhifadhia mafuta katika Bandari ya Mbamba Bay, iliyopo mkoani Ruvuma. Lengo kuu ni kurahisisha usafirishaji wa mafuta kwenda nchi jirani za Malawi na Msumbiji.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo la mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mbamba Bay wenye thamani ya bilioni 75.8, Mwenyekiti wa Bodi, Dkt. Lutengano Mwakahesya, kwa niaba ya Wajumbe wa Bodi, amesema kwamba ujenzi wa matanki hayo utasaidia katika uhifadhi na usafirishaji wa mafuta kwenda katika nchi jirani za Msumbiji na Malawi, yakitokea bandari ya Mtwara kupitia Ziwa Nyasa.

Amesema kuwa ni muhimu kwa TPA kuweka kipaumbele katika ujenzi wa matanki ya kupokelea na kusaidia kampuni za mafuta kupata maeneo ya kuhifadhia mafuta kwa ajili ya kusafirisha kwenda nchi jirani

Meneja wa Mipango ya Mafuta kutoka PBPA Bw. Gilbert Jungulu amesema “matanki hayo yakijengwa kampuni za mafuta zitakuja kwa ajili

ya kuhifadhi mafuta ya kupeleka nchi za jirani na kuingizia kipato mamlaka".

Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhandisi Stella Manyanya ameipongeza Bodi ya PBPA kwa kuona fursa ya ujenzi wa matanki katika bandari hiyo kwani utasaidia kuongeza pato la Taifa na kuongezeka kipato kwa wananchi wa jimbo la Nyasa na kuahidi kutoa ushirikiano kuhakikisha ujenzi wa matanki unafanikiwa.

Naye Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa Manga Gasaya amewashukuru wajumbe wa bodi ya PBPA kwa kuona umuhimu wa kuongeza mradi wa ujenzi wa matanki na kusema kuwa atawasilisha maoni hayo kwenye mamlaka husika na kusisitiza kuwa bado muda upo wa kuongeza ujenzi huo kwenye mradi wa bandari.

Awali, Mhandisi Mkazi wa mradi huo Agathon Mwenda amesema utekelezaji wa ujenzi wa bandari Bandari ya Mbamba Bay utahusisha ujenzi wa gati mbili,ujenzi wa maghala, nyumba za watumishi, jengo la utawala, jengo la abiria, karakana, mnara wa tanki la maji na jengo la huduma za afya.

Amesema ujenzi pia utahusisha barabara za ndani na nje ya bandari kwa ajili ya magari kuingia na kutoka bandarini hapo na ujenzi wa daraja lenye urefu wa mita 105 na upana wa mita 15 kwa ajili ya magari ya kubebea mizigo na eneo la kuhifadhia makontena 3,000 ya mizigo.

Bandari mpya ya Mbamba Bay inajengwa kwenye eneo la pembezoni mwa Ziwa Nyasa, katika Wilaya ya Nyasa, Mkoani Ruvuma. Kazi ya ujenzi wa bandari hii inatekelezwa na mkandarasi Xiamen Ongoing Construction Group Limited, chini ya usimamizi wa mshauri mwelekezi Anova Consult na inatarajiwa kukamilika ifikapo Januari, 2026.

*Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri (PBPA), Dkt. Lutengano Mwakahesya akisalimiana na Mbunge wa Nyasa Mhandisi Stela Manyanya mara baada ya kukamilisha kutembelea ujenzi wa Bandari ya Mbamba Bay iliyopo Wilayani Mbinga.*





*Baadhi ya Wajumbe wa Bodi ya Ushauri wakiongozwa na Mwenyekiti Dkt. Lutengano Mwakahesya (wa kwanza Kulia), CPA Yohana Kilagane (wa pili kulia), Bw. Gilbert Jungulu (wa kwanza kushoto) na Mhandisi Marwa Petro (wa pili kushoto) mara baada ya kumaliza ziara wilayani Mbinga.*

# Watumishi wa PBPA Wapatiwa Mafunzo



*Baadhi ya Watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wakimsikiliza Mkufunzi wa Afya ya Akili Dkt. Garvin Kweka (hayupo pichani) wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi za Wakala jijini Dar es Salaam*

Watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wamepatiwa mafunzo kuhusu Maadili, Rushwa na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ya kutoa Mafunzo ya aina hii kwa watumishi wake.

Mafunzo hayo yalifanyika tarehe Novemba 15, 2025 katika ukumbi wa Mikutano Ofisi ya Wakala yakiwa na lengo la kuwajenga watumishi katika maadili mazuri, kukabiliana na vitendo vya rushwa maeneo ya kazi na namna kujikinga na Magonjwa Sugu Yasiombukiza.

Akizungumza Mwezeshaji wa Mafunzo hayo, Mkuu wa Uelimishaji Umma mkoa wa kiTAKUKURU Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB) Ilala Bi. Grace Mwakyusa amesema lengo ni kukumbushana na kuelimishana kuhusu madhara ya rushwa kwenye jamii na wajibu wa mtumishi wa Umma katika kuzuia na kupambana na rushwa.

Bi. Mwakyusa amesisitiza kuwa malengo mengine ni pamoja na kukumbushana kuwa utumishi ni dhamana ambayo Serikali imewapatia hivyo wanapaswa kuitekeleza kwa uaminifu kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma na sio kufanya kazi kwa maslahi binafsi.

Amesema kuwa, watumishi wa Umma wanapaswa kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa TAKUKURU, pale wanaposhuhudia uwepo wa viashiria au vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa dhidi ya wahusika.

“Kila mtumishi ana wajibu wa kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa mahali pa kazi ili kuhakikisha jitihada za Serikali katika mapambano ya rushwa zinafanikiwa na kuhakikisha rasilimali za taifa pamoja na fedha za Umma zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuleta tija kwa Taifa”, alisisitiza.

Aidha, Mwakyusa amesema kuwa TAKUKURU katika kuzuia rushwa wanafanya tafiti mbalimbali katika maeneo ya kutolea huduma kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa na kushauri taasisi husika namna ya kuziba mianya hiyo.

Kwa upande mwingine, Dkt. Garvin Kweka kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili amewataka watumishi wa Wakala kutenga muda kwa ajili ya masuala mbalimbali yanayohusu maisha binafsi, ili kujiepusha na msongo wa mawazo unaoweza kusababisha matatizo ya afya ya akili.

Dkt. Kweka alisema kuwa, tafiti zilizofanywa na wanasayansi wa afya ya akili, zimebaini kuwa, sababu kubwa za watu kujitoa uhai ni pamoja na mahusiano mabovu au hafifu na jamii zao hivyo kupelekea kuchukua maamuzi yasiyokuwa sahihi.

“Ni muhimu kutenga muda kwa ajili ya familia na jamii ili kuweza kujiepusha na athari zinazoweza kujitokeza kwenye familia ikiwa ni pamoja kutenga muda wa kuwa karibu na watoto”, amesema Dkt. Kweka.

Awali, Bw. Gilibert Jungulu akifungua Mafunzo hayo kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa Wakala amewataka watumishi kuwa wasikivu, kuuliza maswali, kuomba ufafanuzi na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wawezeshaji.

Jungulu amesema kuwa Mafunzo haya ni utekelezaji wa maelekezo ya Serikali kama yalivyoainishwa katika Malengo (a) na (b) katika Mpango Mkakati wa PBPA 2021/22-2025/26 ambayo ni kudhibiti Virusi vya UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasioambukiza na Mapambano dhidi ya Rushwa.

Katika Mafunzo hayo, Grace Mwakyusa kutoka Taasisi ya Kupambana na Rushwa (PCCB) ametoa mada kuhusu Mapambano dhidi ya Rushwa ya Ngono mahala pa kazi, Dkt. Garvin Kweka kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ametoa mada kuhusu uhusiano uliopo kati ya Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza na Afya ya Akili.



*Bi. Grace Mwakyusa, Afisa wa Uhamasishaji Umma wa Mkoa wa Ilala kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB), akitoa mada kuhusu mikakati ya kupambana na rushwa kwa watumishi wa PBPA (hawapo kwenye picha).*



*Baadhi ya Viongozi wakisikiliza mada ya Rushwa wakati wa Mafunzo ya Watumishi wa Ofisi ya Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja(PBPA) yaliyofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi za Wakala jijini Dar es Salaam*

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Mpango akimsikiliza Meneja wa Uendeshaji na Ugavi PBPA alipotembelea Banda la Wakala kwenye maonesho ya kongamano la 10 la Jotoardhi Afrika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam.*

*Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga katika banda la PBPA katika tamasha la KIZIMKAZI linaloendelea Visiwani Zanzibar.*







*Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar Mhe. Zawadi Amour katika banda la PBPA kwenye  Tamasha la Kizimkazi lililofanyika Kusini Unguja, Zanzibar.*



*Mhandisi Issa Mwitazy akitoa elimu kuhusu Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja wa Mafuta (BPS) kwa wanafunzi waliotembelea banda la PBPA katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Dodoma.*

*Picha ya Pamoja ya wafanyakazi wa PBPA waliokuwa washiriki wa Maonesho ya Nanenane jijini Dodoma.*






*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja baada ya ufunguzi wa kikao cha Baraza kilichofanyika jijini Dodoma.*



*Baadhi ya wafanyakazi wa PBPA baada ya ziara ya mafunzo katika ofisi za GBP jijini Dar es Salaam.*




*Baadhi ya wafanyakazi wa PBPA baada ya ziara ya mafunzo katika ofisi za GBP jijini Dar es Salaam.*





PBPA

PETROLEUM BULK PROCUREMENT AGENCY